# Parent Handbook Afterschool 2023-24

Agosti 2023

Wapendwa Wazazi na Walezi wa YouthCity,

Karibuni kwenye programu ya YouthCity 2023-24 ya Baada ya shule! Kwa miezi kadhaa iliyopita, timu zetu zimekuwa zikipanga na kujiandaa kwa programu ya kusisimua iliyojawa na furaha msimu huu wa joto na tuna furaha kuwa nyinyi na familia zenu mmeungana nasi.

Mwaka huu, vijana wa umri wa shule kutoka kote Jiji la Salt Lake waliojiandikisha katika programu ya YouthCity ya Baada ya shule watajihusisha katika shughuli za kielimu za kujifunza kwa vitendo kuchunguza dhana za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (STEM), kujifunza kuhusu afya na ustawi, kujihusisha katika miradi ya huduma kwa jamii, kutembelea vyuo na vyuo vikuu, na kujitengenezea ujuzi wa elimu ya kifedha. Kama zamani, wafanyakazi wa YouthCity wanatengeneza madarasa, shughuli na safari za kwenda maeneo ya kujifunzia zilizoundwa kuchunguza washirika na sehemu za jamii ndani ya jiji letu kubwa, kupanua kujifunza kwa njia zisizo za kitamaduni, kuwapa nguvu vijana kujaribu mambo mapya na kupanua mahusiano yao ya kijamii na makundi rika.Vijana wote watashiriki katika safari za kielimu za kwenda maeneo ya kujifunzia kila wiki pia kuchunguza sanaa na ubunifu, michezo na burudani, ujuzi wa kimaisha na madarasa ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (STEM). Tukijijenga juu ya mafanikio ya mwaka uliyopita, tunayo furaha kuendeleza programu yetu mpya ya uongozi kwa vijana na hivi karibuni tutawatambua watoto 14 kwa ajili ya kuhudumu kwenye Baraza la Uongozi la YouthCity. Unakwenda kuwa mwaka mzuri!

Wafanyakazi wetu wenye mafunzo ya kina, wenye nguvu na upendo wanayo furaha kuanza kufanya kazi na nyinyi na watoto wenu. Hapa chini tumetoa taarifa mtakazozihitaji kuhakikisha tuna mwaka wa shule salama na wa mafanikio. Asanteni kwa kutuamini na watoto wenu na fahamuni kwamba tuna furaha kufanya kazi na kile mmoja wenu. Tafadhali msisite kuwasiliana nasi kadri mtakavyohitaji.

Kila la heri!

ElizabethRich
Mkurugenzi Mshirika Kitengo cha Vijana na Familia
Elizabeth.rich@slcgov.com

## Masaa ya Kazi:

Programu za YouthCity zinafuata kalenda ya Wilaya ya Shule ya Jiji la Salt Lake na huendesha programu kwenye siku ambazo shule iko kwenye kipindi. Wakati shule za Wilaya za Jiji la Salt Lake zimefungwa, hatutoi programu za YouthCity.

Kwa kutumia magari ya jiji, wafanyakazi wa programu huwasafirisha watoto waliosajiliwa kutoka kwenye shule zao hadi kwenye maeneo ya YouthCity. Wakifanya kazi na uongozi wa shule, wafanyakazi husubiri nje ya kila shule kwenye sehemu iliyotengwa. Pindi vijana wote wamehesabiwa, gari litaondoka shuleni na kuwasili YouthCity.

Wazazi/Walezi wanawajibika kuwachukuwa watoto wao kutoka YouthCity kila siku. Vijana wote wanatakiwa kuchukuliwa saa 12:00 jioni kila usiku. Wazazi wanaweza kusema kwenye fomu ya usajili kuwa watoto wao wanaweza kujitoa wenyewe na kutoka kwa programu na/au watu wazima wengine ambao wanaweza kuwachukua kutoka kwenye programu.

## Tarehe Muhimu:

| | |
|---|---|
| Jumanne, Agosti 22 | Siku ya Kwanza ya Programu yaYouthCity ya Baada ya shule 2023-24 |
| Jumatatu, Septemba 4 | Siku ya Wafanyakazi – Hakuna YouthCity |
| Oktoba 12-13 | Mapumziko Msimu wa Vuli – HakunaYouthCity |
| Jumatatu, Oktoba 16 | Hakuna Shule – HakunaYouthCity |
| Novemba 22-24 | Mapumziko ya Shukrani – HakunaYouthCity |
| Desemba 21 - Januari 3 | Mapumziko Msimu wa Baridi – HakunaYouthCity |
| Jumatatu, Januari 15 | Siku ya MLK – Hakuna YouthCity |
| Jumatatu, Februari 19 | Siku ya Maraisi – HakunaYouthCity |
| Aprili 1-5 | Mapumziko Msimuwa Masika – HakunaYouthCity |
| Ijumaa, Mei 24 | Siku ya Mwisho ya Programu ya YouthCity ya Baada ya shule 2023-24 |

*Kalenda ya YouthCity inaweza kubadilishwana wazazi na walezi wote watataarifiwa kadiri ya mabadiliko.*

## Mawasiliano ya Programu:

| Programu za YouthCity | Uongozi wa Eneo la YouthCity | Simu | Barua pepe |
|---|---|---|---|
| Central City | Erica Andino | 801-381-6836 | Erica.Andion@slcgov.com |
| Fairmont Park | Lauren Underwood | 801-573-6519 | Lauren.underwood@slcgov.com |
| Fairpark | Angel Gomez | 385-495-8960 | Angel.Gomez@slcgov.com |
| Liberty Park | Jess Ung | 801-558-8223 | Jess.Ung@slcgov.com |
| Ottinger Hall | Connie Paredes-Poza | 801-573-1349 | Connie.paredes-pozas@slcgov.com |
| Sorenson Unity 3-6 | Lola Paredes | 801-879-9678 | Dolores.Paredes@slcgov.com |
| Sorenson K-2 | Fernando Puga–Interim | 385-495-8960 | Fernando.Puga@slcgov.com |

## Programu ya Baada ya shule 2023-24

Kama katika miaka iliyopita, YouthCity itatoa juzi mbalimbali zinazorandana na umri kulingana na shughuli za kujifunza kwa vitendo zilizojikita kwenye Sanaa na Ubunifu, Michezo na Burudani, Juzi za Maisha, STEM na uchunguzi wa mazingira ya nje. Madarasa na shughuli hizi vimeundwa ili kusisimua kujifunza na kutengeneza mahusiano ndani ya jamii.

Mwaka huu wa shule tuna furaha kulenga kujifunza kwetu kwenye mada zifuatazo za kipindi:

| Tarehe | Mada ya Kipindi | Eneo la Kulenga la Kujifunza Hisia za Kijamii | Klabu ya Huduma ya Wafanya Mabadiliko wa YouthCity |
|---|---|---|---|
| Wiki ya Ukaribisho Agosti 21 - Septemba 1 | Utambulisho | Je! Nguvu ya Mmoja ni ipi? | Kuchagua Wanabaraza wa Uongozi wa YouthCity Msimu wa Vuli 2023 |
| Msimu wa 1 wa Vuli 2023 Septemba 5 - Oktoba 20 | Mkutano wa Kisayansi | Uanuwai na Ujumuisho<br><br>UthabitinaHaki ya Kijamii | Mradi Mkubwa wa Huduma ya Programu ya Kusafisha Mazingira |
| Msimu wa 2 wa Vuli 2023 Oktoba 23 - Desemba 20 | Jikite kwenye Afya | HurumanaKufikiri kwa Umakinifu<br><br>Kujitambua na Huruma | Mradi wa Huduma ya Afya na Ustawi Eneo husika |
| Msimu wa Baridi 2024 Januari 8 - Machi 22 | Kipindi cha Huduma<br><br>Mkataba wa Haki wa Watoto kwenye Mazingira ya Nje | Mawasiliano naUtatuaji Tatizo<br><br>Utumishi na Huduma | Siku ya Huduma ya MLK |
| Msimu wa Masika 2024 Machi 25 - Mei 24 | Chuo Kikuu cha YouthCity<br><br>CityVille | Utatuaji Tatizo na Mahusiano ya Vijana<br><br>Ubunifu,Diplomasia na Udadisi | Mradi wa Huduma ya Afya na Ustawi Eneo husika |

## Safari za kwenda Maeneo ya kujifunzia:

Kila wiki, vijana watatembelea nyumba mbalimbali za makumbusho, biashara, na vivutio kusaidia kutengeneza mahusiano yenye maana na jamii yetu. Wafanyakazi wa programu wamepanga na kubuni kwa umakini mitoko hii lengwa kuwasaidia watoto wa YouthCity kutengeneza mahusiano ya kitaaluma, kujenga urafiki, na kujenga ujuzi wa kutatua matatizo kulingana na umri husika. Tahadhari zote za kiafya zitafuatwa kusaidia kuwaweka salama washiriki wa programu, wafanyakazi wa programu, na wanajamii. Meneja wa Programu za Jamii za kila mwezi watazipa familia kalenda ya matukio ikihusisha safari za kwenda maeneo ya kujifunzia na shughuli.

## Gharama za Programu:

Gharama za programu zinaamuliwa kulingana na ukubwa wa familia na kipato. Tafadhali tazama kifurushi cha usajili kwa taarifa zaidi. Gharama zote za programu ambazo hazijalipwa lazima zilipwe zote kabla ya mwanafunzi kuweza kuhudhuria programu hii. Kama tahadhari ya kiafya, tunahamasisha familia zote zilipie gharama za programu mtandaoni. Cheki au oda za pesa zitakubaliwa kadri itakavyohitajika. Meneja Wakuu wa Programu ya Jamii na Meneja wa Programu za Jamii watakuwa wakiwasiliana na familia wakiwa na taarifa kuhusu gharama zozote za programu ambazo bado hazijalipiwa.

## Miongozo ya Kiafya na Usafi:

IKulingana na miongozo ya kiafya na kiusalama iliyotolewa na Idara ya Afya ya Utah, tahadhari zifuatazo za kiafya zitahusishwa katika programu hii ya YouthCity 2023-24 ya Baada ya shule. Vijana ambao hawafuati miongozo hii wataondolewa kwenye programu.

Wafanyakazi wa programu watafuata ratiba madhubuti ya usafi ili kunadhifisha kuta na sakafu za jengo siku nzima. Kila kituo kitafanyiwa usafi mkubwa kila siku baada ya masaa ya programu. Milango ya jengo itafungwa wakati wa masaa ya programu.

## Kunawa mikono:

Unawaji mikono endelevu na wa mara kwa mara unahusishwa katika siku yote na kuhamasishwa wakati wa mapumziko na mida ya kubadilishana. Watu wote watakuwa wakinawa mikono wanapoingia kwenye jengo, wanapotumia vyoo, na kabla ya milo yote na vitafunwa.

## Usafishaji na Uuaji vijidudu:

Maeneo yote ya YouthCity yana vifaa vya kusafishia na kutakasa ili kuhakikisha kuta na sakafu zinazoguswa sana zitakuwa zinasafishwa na kutakaswa baada ya kila zinapotumika. Tumeweka ratiba kwa ajili ya uuaji vijidudu na utakasaji wa maeneo yetu ambayo itafuatwa kabla ya programu, wakati wa programu, na baada ya programu. Vijana wataalikwa kusaidia kuweka maeneo haya kuwa masafi na nadhifu. Majengo yote ya YouthCity yatafanyiwa usafi mkubwa na vijidudu kuuliwa pindi programu inapoisha kila usiku.

## Sera ya Ugonjwa:

Ikiwa mtoto wako hajihisi vizuri, atapaswa kubakia nyumbani na kutokuhudhuria programu. Kama mtoto ataonesha dalili wakati wa programu, wafanyakazi watamtenga mtoto na wenzake kwa usalama na kutoa huduma ya kwanza na uangalizi, kuwasiliana na wazazi na kuomba kwamba mtoto achukuliwe kutoka kwenye programu mapema iwezekanavyo. Uongozi wa Programu utafanya kazi na wazazi kufuatilia afya na dalili za mtoto kufahamu ni wakati gani mtoto anaweza kujiunga tena na YouthCity. Ikiwa mtoto wako haudhurii shule kutokana na ugonjwa atapaswa kutokuhudhuria YouthCity. Tafadhali wasiliana na Meneja wa Programu za Jamii kuripoti ikiwa mtoto wako hatoudhuria programu.

## Itifaki za Uviko 19:

Kulingana na maelekezo kutoka uongozi wa Jiji, vijana na wafanyakazi watafuata miongozo ya afya inayopendekezwa kusaidia kudumisha afya na usalama ndani ya jamii yetu. Vijana na wafanyakazi wanaweza kuchagua kuvaa barakoa na YouthCity itatoa barakoa kadri inavyohitajika. Taarifa na maelekezo zaidi yatatolewa kadri inavyohitajika.

## Skuta, Baiskeli, na Upatikanaji wa Viwanja vya michezo:

Vijana wanaweza kuendesha baiskeli au skuta wakati wa masaa ya programu ya YouthCity. Wakati wa masaa ya programu vijana watahitajika kuvaa kofia ngumu wakati wakiendesha baiskeli, vibao mtelezo, au skuta. Kwa nyongeza, vifaa vya viwanja vya michezo vitaruhusiwa ili mradi mandhari za kiafya za jamii zinadumishwa.

## Wafanyakazi na Mtindo wa Kupata wafanyakazi wa YouthCity:

Wafanyakazi wote wa YouthCity hupokea mafunzo ya masaa 20 kwa kiwango cha chini kwa mwaka. Mafunzo haya yanahusisha makuzi ya vijana balehe, huduma ya kwanza, CPR, mazoea yanayofaa kinidhamu, utunzaji chakula, mafunzo ya gari, uendeshaji wa kujilinda, uzuiaji unyanyasaji wa watoto, na mazoea bora katika utengenezaji wa mitaala. Wafanyakazi hutengeneza mitaala kulingana na usuli na uzoefu wao. Wafanyakazi wote wamekamilisha ukaguzi mkali uliyofanywa na Ofisi ya Utoaji Leseni za Uangalizi wa watoto.

## Kumleta na Kumchukuwa Mtoto Wako:

Kila eneo la YouthCity lina muundo na mpangilio wa kipekee wa programu. Tafadhali wasiliana na Meneja wa Programu za Jamii mwenye jukumu hilo ili kupata maelekezo na itifaki za kuegesha magari kwa eneo husika. Wafanyakazi wa YouthCity wanawajibika kwa watoto walioandikishwa katika programu pindi kengele ya shule inapolia. Vijana wote ni lazima wachukuliwe ifikapo saa 12:00 jioni kila siku. Tafadhali onesha kwenye kifurushi cha usajili ni watu gani wana mamlaka ya kumchukuwa mtoto wako kutoka YouthCity. Wafanyakazi wa Programu wana mafunzo tu ya kuwakabidhi vijana kwa watu waliopewa mamlaka walioorodheshwa katika fomu ya usajili.

## Mawasiliano ya Dharura:

Wazazi/Walezi ni lazima watoe majina ya watu wote waliopewa mamlaka ya kuwachukua watoto wao, fomu ya kuondoka imeambatanishwa katika nyaraka zetu za usajili. Tafadhali hakikisha unawaorodhesha watu wote ambao wana mamlaka ya kumchukuwa mtoto wako na kuhakikisha wanaelewa itifaki za kumchukuwa zilizonotiwa hapo chini. Watu wazima ambao hawatambuliki wataombwa vitambulisho.

## Chakula na Lishe:

YouthCity itatoa kitafunwa chenye afya kila siku. Menyu zinachapishwa ndani ya kila eneo na zinaweza kupatikana pindi zikiombwa. Wazazi pia wanaweza kutuma kitafunwakwa ajili ya watoto wao kila siku. Tafadhali hakikisha chakula kiko tayari kuliwa na HAKIHITAJI kuwekwa kwenye jokofu/friji au maikrowevu. Tunaomba pia chakula cha wanafunzi wako kiwekewe alama ya majina yao. Wanafunzi wanapaswa kuja na chupa ya maji kila siku.

Ni wajibu wa mzazi/mlezi kuitaarifu programu ikiwa mtoto wake ana mizio yoyote ya chakula. Programu itatoa chaguo zinazofaa za vitafunwa kwa wale wenye mahitaji maalum ya kimlo. Tafadhali onesha kwenye fomu ya usajili vyakula ambavyo mwanao hatumii na ana mzio navyo.

## Ugonjwa:

Vijana wenye yoyote kati ya dalili zifuatazo, hawapaswi kuhudhuria Programu:

- Homa
- Kikohozi
- Kubana kwa pumzi
- Kuharisha
- Kutapika
- Mafua makali na/au vidonda vya koo
- Joto la mwili kubwa zaidi ya nyuzi 99
- Watoto na watu wazima wenye yoyote kati ya dalili hizi wasiingie kabisa kituoni na wawasiliane na mtoa huduma wao wa afya kuona kama dalili hizi zinahusiana na UVIKO-19 au ugonjwa mwingine wowote. Ikiwa yoyote anayehusiana na kituo, mwanafunzi au mfanyakazi akigundulika kuwa na UVIKO-19, kituo chetu kitahitaji kufungwa kwa muda.

Ikiwa mwanafunzi wako akionesha dalili za ugonjwa baada ya kuwasili kituoni, tutamtenga na vijana wengine. Mtoto wako atakuwa akitazamwa kwenye eneo tulivu. Ikiwa mwanafunzi wako atakuwa mgonjwa wakati wa muda wa programu, Uongozi wa Programu utawasiliana na wewe na kukuhitaji wewe au mtu uliyempa mamlaka kuja kumchukua mtoto wako kutoka kwenye programu haraka. Ikiwa mzazi hawezi kupatikana, namba za mawasiliano ya dharura za kijana zitapigiwa.

## Majeraha:

Wafanyakazi wote wa YouthCity wana mafunzo katika Huduma ya Kwanza na CPR. Katika kesi za majeraha ambayo yanaonekana kuwa madogo kwa asili, huduma ya kwanza itatolewa kwenye mazingira husika. Katika kesi ambazo ni kubwa zaidi, tutamjulisha mzazi haraka iwezekanavyo. Ikiwa ni muhimu, tutawapigia au kuwasiliana na watu wengine wazima kwenye orodha ya mawasiliano ya dharura. Wafanyakazi watatenda kulingana na uamuzi wao bora kwa ajili ya ustawi wa mtoto. Hii inaweza kuhusisha lakini haiishii kwenye: kuita gari la wagonjwa au kufanya CPR au tekniki nyingine za Huduma ya Kwanza.

## Dawa:

YouthCity haitoi dawa zozote kwa washiriki waliojiunga.

## Chanjo:

Kila mtoto anahitajika kuwa na chanjo za wakati wa sasa.

## Matarajio ya Tabia:

YouthCity inatarajia watoto kuwa na heshima na kuwajibika wakati wakiwa kwenye programu. Tunatarajia kwamba watoto watawaheshimu wanafunzi wengine, wafanyakazi na watu wazima wengine, vifaa, malighafi, na wao wenyewe. Ikiwa vijana hawawezi kufuata matarajio haya, wafanyakazi wa programu watatengeneza adhabu inayofaa kufifisha tabia husika.

Pindi tabia isiyofaa ikiendelea kukua watoto watapewa onyo la mdomo na wafanyakazi watairekebisha tena tabia yake kwenye chaguo lenye tija zaidi. Ikiwa tabia hii hasi ikiendelea, adhabu ya ziada italazimika. Adhabu hiyo inatofautiana kutoka kutolewa kwa muda mfupi, kwa muda mrefu kutoka kwenye shughuli husika au darasa, kupoteza mapendeleo mengine ya programu au kikao na mzazi au mlezi wa mwanafunzi.

Katika nyakati ambapo tabia hasi inaendelea kwa kipindi kirefu zaidi cha muda, mwanafunzi anaweza kusimamishwa kwa muda kutoka kwenye programu au katika kesi kubwa, kuondolewa kabisa. Usimamishwaji wa muda unatofautiana kutoka siku 1 hadi 5. Kabla ya kusimamishwa kwa muda, Uongozi wa Programu, mwanafunzi, na mzazi watakutana na kufikia mpango wa usimamishwaji wa muda unaokubalika. Kikao na Meneja Mkuu wa Programu ya Jamii wa eneo husika kinahitajika kabla ya mwanafunzi kuweza kurudi kwenye programu.

Katika kesi hizi kubwa, YouthCity ina haki ya kumsimamisha kwa muda au kumuondoa kabisa mshiriki.

Programu za YouthCity HAZINA KABISA uvumilivu kwenye ukatili. Katika kesi za ukatili, vitisho vya ukatili, na uonevu, wanafunzi wanaweza kusimamishwa au kuondolewa kabisa papo hapo. Wazazi watapigiwa simu na kuombwa kuja kuwachukuwa wanafunzi wao haraka iwezekanavyo. Unyanyasaji wa kijamii, utengaji, au unyanyasaji wa kimtandao kupitia mitando ya kijamii vitazingatiwa kwa ukubwa kama unyanyasaji wa kikatili na vinaweza kuwa ni sababu za kusimamishwa kwa muda au kuondolewa kabisa.

## Vitu Vya Kuchezea, Vitu Binafsi, na Simu za Mkononi:

YouthCity itatoa shughuli, chakula, mahitaji, na vifaa kwa washiriki wote. Hatukubali kuwajibika kwenye Vituvya kuchezea, vitu binafsi, na Simu za Mkononi: au vifaa vya kubebeka vya kuchezea kutoka nyumbani. Programu yetu ipo katika muundo kiasi kwamba kuna muda au hitaji dogo sana kwa mtoto kujivuruga na mfumo wa kuchezea au kucheza muziki kutoka nyumbani. Wakati hatuwezi kukataza wanafunzi kuja na simu za mkononi kwenye programu, tuna sheria kali kuhusu jinsi simu zinavyotumika kwenye programu yetu. Sera yetu ni kwamba hazitakiwi kutumika wakati wa masaa ya darasa na, wanafunzi watapewa onyo na halafu wataombwa kuzipeleka ofisini kwa muda wa siku uliosalia. Wazazi wanaweza kuwasiliana nawanafunzi wao kupitia simu yetu ya programu na wanafunzi wanaweza kuwasiliana na wazazi kwa kutumia simu ya mkononi ya programu kadri inavyohitajika.

Ikiwa wanafunzi wataleta vitu binafsi kwenye programu, tafadhali hakikisha ni vifaa au mahitaji tu ambayo ni rahisi kutakasa. Tunataka kuhakikisha tunafuata itifaki zote za usalama zilizoundwa na programu. Hakuna vitu binafsi vinavyoweza kuachwa kituoni usiku mzima na wanafunzi wote wanatakiwa kwenda nyumbani na mali zote binafsi mwisho wa siku au kuziweka hatarini kutupwa.

## Je! Nije na nini kutoka nyumbani?

Washiriki wote walioandikishwa watapewa kabati na au sehemu ya kuweka vitu vyao binafsi. Ili kuhakikisha msimu wa joto salama na wenye mafanikio tunapendekeza vijana waje na vitu vifuatavyo ambavyo vinaweza kubakia kwenye programu kwa muda wote wa msimu wa joto.

- Nguo za kubadilisha ambazo zinaweza kubakia YouthCity... katika kesi za dharura
- Shati la rangi
- Nguo za hali ya hewa ya kimsimu kadri inavyohitajika

## Unyanyasaji/Kutelekezwa:

Tukiwa kama wataalamu wa huduma ya watoto, tunaamriwa na sheria kuripoti kesi zozote tunazohisi ni za unyanyasaji au utelekezaji wa mtoto. Hatutasita kuomba msaada kwa ajili ya mtoto yoyote.

## Sera ya Malalamiko:

Kama mshiriki wa programu, mzazi, au mlezi ana tatizo na programu ya baada ya shule ya YouthCity au mfanyakazi, utaratibu ufuatao wa malalamiko unapaswa kutumiwa. Ikiwa ni sawa, tafadhali jadili tatizo hilo na Meneja Mkuu wa Programu ya Jamii kwanza. Ikiwa hauwezi kujadili tatizo hilo na uongozi wako wa programu kwa eneo husika, au hauwezi kufikia suluhisho, tafadhali wasilisha tatizo lako kwa maneno ya mdomo au katika maandishi kwa Mkurugenzi Mshirika wa Vijana na Familia. Mkurugenzi Mshirika atawasiliana na wewe kujadili matatizo hayo na wewe pamoja na wafanyakazi wanaohusika kupata suluhisho. Ikiwa tatizo lako halijasuluhishwa kukuridhisha, au kama una tatizo kumhusu Mkurugenzi Mshirika wa programu, unaweza kuwasilisha tatizo lako kwa maneno ya mdomo au katika maandishi kwa Mkurugenzi wa Kitengo cha Vijana na Familia Jiji la Salt Lake. Mkurugenzi wa Kitengo atajadili tatizo hilo na wewe na wafanyakazi wanaohusika kupata suluhisho. Ikiwa tatizo lako halijasuluhishwa kukuridhisha, au kama una tatizo kumhusu Mkurugenzi wa Kitengo, unaweza kuweka matatizo yako katika maandishi kwa Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Jamii na Vitongoji Jiji la Salt Lake. Naibu Mkurugenzi atafanya uamuzi wa mwisho kuhusu jinsi suala hilo litakavyosuluhishwa na kutuma barua pepe kwa mshiriki.